




JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA
TUME YA VYUO VIKUU TANZANIA



Dar es Salaam, 8 Julai, 2022

TAARIFA KWA UMMA

KUFUNGULIWA KWA DIRISHA LA UDAHILI KWA WAOMBAJI WA SHAHADA YA KWANZA KATIKA TAASISI ZA ELIMU YA JUU KWA MWAKA WA MASOMO 2022/2023

1.0 Utangulizi

Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU) inapenda kufahamisha umma, Taasisi za Elimu ya Juu na Wadau wote wa Elimu ya juu ndani na nje ya nchi kuwa kufuatia kutangazwa kwa matokeo ya Mtihani wa Kidato cha Sita, Tume imefungua dirisha la maombi ya udahili kwa waombaji wa Shahada ya Kwanza **kuanzia leo tarehe 8/7/2022** badala ya tarehe 15/7/2022 iliyokuwa imepangwa awali. Dirisha hili litakuwa wazi hadi tarehe **05/8/2022**.

Tume inawahimiza waombaji wote wa udahili kuendelea kupata taarifa sahihi kupitia tovuti ya TCU www.tcu.go.tz, tovuti za vyuo vilivyoruhusiwa kudahili wanafunzi wa Shahada za Kwanza, pamoja na taarifa mbalimbali zinazotolewa na TCU kupitia vyombo vya habari.

Vile vile, Tume inatoa wito kwa waombaji wa udahili na wananchi kwa ujumla kuhudhuria **Maonesho ya 17 ya Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia** yatakayofanyika katika Viwanja vya Mnazi Mmoja, Dar es Salaam ambapo watapata fursa ya kuonana ana kwa ana na Vyuo vya Elimu ya Juu. Maonesho hayo yatafanyika kuanzia **Julai 18 hadi Julai 23, 2022**.

2.0 Utaratibu wa Kutuma Maombi ya Udahili kwa Mwaka wa Masomo 2022/2023

2.1 Makundi ya Waombaji wa Udahili

Maombi ya Udahili wa kujiunga na Shahada ya Kwanza yanahusu makundi matatu ya waombaji:

- Wenye sifa stahiki za Kidato cha Sita;
- Wenye sifa stahiki za Stashahada (Ordinary Diploma), au sifa linganifu; na
- Wenye sifa stahiki za Cheti cha Awali (Foundation Certificate) ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Ili kufahamu sifa stahiki kwa makundi matatu yaliyotajwa hapo juu, waombaji wanaelekezwa kusoma vigezo vilivyooneshwa katika vitabu vya mwongozo vya TCU (**Undergraduate Admission Guidebooks for 2022/2023**) vinavyopatikana katika tovuti ya TCU www.tcu.go.tz.

2.2 Utaratibu wa Kutuma Maombi ya Udahili

- a) Maombi yatumwe moja kwa moja kwenye vyuo ambavyo muombaji amevichagua na kuchagua programu za masomo anazozipenda. Mwongozo wa programu zilizoidhinishwa kudahili na vigezo stahiki (**Undergraduate Admission Guidebooks for 2022/2023**) unapatikana kwenye tovuti ya TCU www.tcu.go.tz.
- b) Maelekezo mahsusi ya jinsi ya kutuma maombi yanatolewa na vyuo husika.

2.3 Vigezo na Sifa za Waombaji Udahili

Vigezo na sifa katika programu mbalimbali za masomo vinapatikana katika vitabu vya mwongozo vya TCU (**Undergraduate Admission Guidebooks for 2022/2023**) kwenye tovuti ya TCU www.tcu.go.tz.

2.4 Masuala Muhimu ya Kuzingatiwa na Waombaji

- a) Kusoma mwongozo wa udahili uliotolewa na TCU kwa makini na kuelewa kabla ya kuanza kutuma maombi yoyote ya udahili;
- b) Kuingia katika tovuti za vyuo ili kujua taratibu za kutuma maombi;
- c) Kutuma maombi moja kwa moja vyuoni kupitia mifumo ya kielektroniki iliyowekwa na vyuo husika;
- d) Kuwasiliana na vyuo moja kwa moja na kupata taarifa za kina kuhusu programu za masomo ili kujiridhisha kabla ya kutuma maombi; na
- e) Waombaji wenye vyeti vilivyotolewa na mabaraza ya mitihani nje ya nchi ni lazima wawasilishe vyeti vyao Baraza la Mitihani la Tanzania (NECTA) kwa vyeti vya Elimu ya Sekondari au Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi (NACTVET) kwa vyeti vya Stashahada ili kupata ithibati ya ulinganifu wa sifa zao kabla ya kutuma maombi ya udahili.

3.0 Tahadhari

Tume inatoa wito kwa waombaji wote wa Shahada ya Kwanza, endapo watahitaji kupata ufafanuzi wa suala lolote linalohusu udahili, wawasiliane moja kwa moja na vyuo husika. Aidha, iwapo watahitaji maelezo ya jumla wanaweza kuwasiliana na TCU kwa kutumia barua pepe es@tcu.go.tz.

TCU inawaasa wananchi kuepuka kupotoshwa na watu wanaojiita mawakala au washauri wanaodai wanatoa huduma ya jinsi ya kujiunga na vyuo vya elimu ya juu hapa nchini.

Imetolewa na:



Prof. Charles D. Kihampa
KATIBU MTENDAJI
TUME YA VYUO VIKUU TANZANIA



Jiandae Kuhesabiwa Siku ya Jumanne tarehe 23 Agosti, 2022